# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Mtaa wa Posta,**

**S.L.P. 2599,**

**33101 MWANZA,**

**Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.**

**www.pccb.go.tz**

**MWANZA – APRILI, 2022**

## TAKUKURU MWANZA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 25. MRADI MMOJA WACHUNGUZWA

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Miradi ya maendeleo endelevu inategemea rasilimali fedha, bidhaa, nguvu kazi , mawazo na ushiriki wa dhati na uadilifu wa kila mwananchi. Ukosefu wa uwazi na uwajibikaji imekuwa ni changamoto na kupelekea kuwepo kwa vitendo vya rushwa kwenye shughuli za utekelezaji wa miradi.

Katika kuhakikisha vitendo vya rushwa vinazuiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kunakuwepo na uwajibikaji kwa watendaji, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwezi Januari-Machi 2022, imefanya ukaguzi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa **miradi ya maendeleo 17** yenye thamani ya **Sh. Bil 25,650,415,420/=**

Kati ya miradi hiyo 17 iliyokaguliwa, miradi ya elimu 6 ilihusu ujenzi wa matundu ya vyoo na ujenzi wa vyumba vya madarasa yenye thamani ya Sh. 7,013,490,626/=; miradi 8 ilihusu ujenzi na ukarabati wa Barabara yenye thamani ya Sh. 2,613,257,660/=, mradi 1 ni wa ujenzi wa stendi ya

mabasi Nyegezi uliopo katika Halmashauri ya jiji la Mwanza wenye thamani ya Sh. 15,885,589,063/= na miradi 2 ni ya ufuatiliaji wa fedha za UVICO kwa wilaya ya Nyamagana na ngazi ya Mkoa Sh. 138,078,071/=. Kati ya miradi hiyo iliyokaguliwa miradi 6 imekamilika na miradi 11 inaendelea na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha TAKUKURU imeanzisha uchunguzi wa mradi wa matundu 31 ya vyoo katika shule ya msingi Sengerema wenye thamani ya Sh. 16,004,000/= baada ya kuwepo kwa tuhuma ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi na changamoto ya usimamizi wa mradi.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Pamoja na miradi hiyo iliyokaguliwa, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imeweza kufanya Uchambuzi wa mfumo wa Usimamizi wa Mapato yatokanayo na madini ya Ujenzi, Uchambuzi wa mfumo wa Mianya ya rushwa katika utoaji elimu ya Ugani kwa wakulima, Uchambuzi wa mfumo na mianya ya rushwa katika utekelezaji wa shughuli za chanjo ya uviko-19, Uchambuzi wa mfumo wa utendaji kazi wa wakala wa huduma za ufundi na umeme:TEMESA, Uchambuzi wa mfumo wa mradi wa ujenzi wa vyoo katika shule za msingi na maeneo ya umma, Uchambuzi wa mfumo – tathmini ya utendaji kazi wa wakala wa huduma ya ununuzi serikalini (GPSA) , Uchambuzi wa mfumo wa matumizi ya asilimia 10 zinazotengwa na Halmashauri kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji mapato katika kivuko cha Kigongo-Busisi.

Kupitia chambuzi za mifumo zilizofanyika kwenye maeneo mbalimbali, zipo changamoto ndogo zilizobainika kwa kila chambuzi, hivyo vikao vya warsha vimefanyika kwa lengo la kujadili kwa pamoja na wahusika ili kuwekeana maazimio na makubaliano ya pamoja kwa ajili ya utekelezaji kwa yote yaliyobainika ili kuboresha mifumo na utoaji wa huduma.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Kwa upande wa Elimu kwa Umma katika kipindi cha Januari-Machi 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imetoa elimu na kuyafikia makundi mbalimbali kwa kufanya semina 23, mikutano ya hadhara 42, vipindi 4 vya redio, uandishi wa habari 10 na kuimarisha klabu za wapinga rushwa 128 kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo.

Vilevile, TAKUKURU Mkoa wa mwanza imefanya maonesho 9 ikiwemo maonesho katika wiki ya sheria, onesho kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake lililofanyika kimkoa katika viwanja vya Nyamagana jijini Mwanza ambapo watu 418 wakiwemo wanawake, vijana na wazee walielimishwa kuhusu haki na wajibu wao katika kuleta maendeleo endelevu pamoja na kuepuka rushwa ya ngono kwa kuvunja ukimya na kutoa taarifa TAKUKURU. Kauli mbiu katika maadhimisho hayo "Kukuza kizazi cha haki na usawa kwa maendeleo endelevu".

Aidha katika kipindi hicho mkazo zaidi wa elimu umetolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao pamoja na utekelezaji wa mkakati wa pamoja wa TAKUKURU na SKAUTI wenye kauli mbiu **TAKUSKA –TOKOMEZA RUSHWA** wenye lengo la kushirikisha vijana wa Skauti kwenye kuzuia na kupambana na Rushwa.

TAKUKURU Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha Januari- Machi imeendelea na utekelezaji wa mkakati huo ambapo kwa wilaya ya Nyamagana na Wilaya ya Magu mafunzo yametolewa kwa walimu walezi 203 wa SKAUTI, viongozi 28 wa idara ya elimu na viongozi 80 wa Skauti.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwa na uelewa wa pamoja wa mambo mbalimbali yahusuyo kukemea na kuzuia rushwa ili nao waweze kuwaelimisha vijana wa Skauti waliopo mashuleni.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Kwa upande wa kazi za Uchunguzi, TAKUKURU Mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2022 imepokea **taarifa 132.** Kati ya taarifa hizo,**taarifa 89 zinahusu vitendo vya rushwa** na **taarifa 43 hazikuhusu vitendo vya rushwa.** Kwa taarifa **89** zilizohusu rushwa tumefungua majalada ya uchunguzi ambapo majalada **22** uchunguzi wake umekamilika (na jalada **1** limefungwa kwa kukosa ushahidi). Vilevile majalada **67** uchunguzi wake bado unaendelea.

Aidha kwa **taarifa 43 zisizohusu** rushwa taarifa 10 zimehamishiwa katika idara zingine na taarifa 33 wahusika wameelimishwa na kushauriwa. Katika kipindi hicho TAKUKURU Mkoa wa Mwanza imefungua kesi mpya 8, imeshinda kesi 2 kati ya kesi 2 zilizotolewa maamuzi mahakamani na kwa sasa kuna kesi 19 zinazoendelea Mahakamani.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**
TAKUKURU inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na mkakati uliopo kwa kipindi cha Aprili -Juni, 2022 ni kuendelea kusimamia kwa karibu zaidi, matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuendelea kushirikiana kwa ukaribu na wadau wetu ili kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa mkoani kwetu.

Elimu itatolewa zaidi kwa utaratibu wa TAKUKURU MOBILE, yaani TAKUKURU inayotembea ili kuhakikisha kuwa TAKUKURU inawafikia wananchi moja kwa moja katika maeneo yao na kuwaelimisha juu ya umuhimu na wajibu wao katika kusimamia miradi ya maendeleo kwani tunaamini njia hii pia itaongeza wigo wa ushirikishwaji wa wananchi kwenye Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

**Wito kwa wananchi;**

Ninawaomba wananchi wa Mkoa wa Mwanza waendelee kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa ili tuweze kuwachukulia hatua wahusika kwa mujibu wa sheria.

**Mwisho,** wimbi la matapeli wanaojifanya kuwa ni maafisa wa TAKUKURU bado lipo, hivyo ninawatahadharisha wananchi wa Mkoa wa Mwanza pindi mwananchi unapopigiwa simu na kuombwa pesa ili ushughulikiwe jambo lako ambalo unaambiwa liko TAKUKURU tafadhali toa taarifa kwa kupiga simu au fika ofisini mara moja.

***KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LANGU***

**“Kwa taarifa za vitendo vya rushwa tafadhali fika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu nawe au piga simu ya dharura namba 113 au tuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au Piga *113# fuata maelekezo” Huduma hii ni ya BURE.**

**IMETOLEWA NA:**

**FRANK MKILANYA - 0738 150 162**
**MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA**